

MKATABA WA UPANGAJI

MKATABA huu umetayarishwa leo tarehe 25 mwezi 09.mwaka 2025

KATI YA

JAPHARI MURRO wa Arusha Tanzania (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **"MWENYE ENEO"**) kwa upande mmoja.

TARMALS AGRO LIMITED wa Dar es salaam (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **"MPANGAJI"** kwa upande mwingine.

NA KWA VILE Mwenye ENEO amekubali kupangisha na Mpangaji amekubali kupangishwa sehemu ya eneo la kiwanda lenye ukubwa wa **Heka 20** lililopo **ARUSHA** Mtaa wa **KISONGO KARIBU NA KASONGO PRISON MKOA WA ARUSHA TANZANIA**

HIVYO BASI Makubaliano hayo yameshuhudia yafuatayo:-

1. MUDA WA MKATABA

Mkataba huu utakuwa wa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe 25 Mwezi 09 mwaka 2025 na utamalizika tarehe 24 mwezi 09 mwaka 2030.

2. KODI

Mwenye eneo amekubali kupangisha na mpangaji amekubali kupangishwa katika sehemu hiyo ya eneo la kiwanda kwa madhumuni ya kufanya biashara kwa kulipa kodi ya **Shilingi Milioni Tatu (3,000,000)** kwa mwezi mmoja. Wakati wa kutiliana saina mwenye eneo amekubali kupokea **Tsh Milioni Mia Moja na Themanini Tu (180,000,000)** Ikiwa ni malipo ya miaka mitano.

3. NI WAJIBU WA MPANGAJI KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- Kutopangisha Mtu mwingine katika eneo hilo bila idhini ya Maandishi ya Mwenye eneo
- Kulipia gharama zote za umeme katika eneo hilo kwa kipindi cha Mkataba.
- Kuweka eneo na mazingira yake katika hali ya usafi na kufanya matengenezo madogo madogo inapobidi na gharama za matengenezo kwa matumizi yake hazitakuwa jukumu la Mwenye eneo
- Iwapo makubaliano hayo hayataongezwa muda wake, atamkabidhi Mwenye eneo sehemu hiyo ikiwa tupu.

4. NI WAJIBU MWENYE ENEO KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- Kuweka eneo katika hali nzuri
- Kutombughudhi Mpangaji wa eneo hilo anayesimamia kwa masharti yaliyopo.

5. INAKUBALIWA PIA KUWA

- (a) Endapo Mpangaji atakuwa na Nia ya kuendeleza atawajibika kutoa taarifa ya Maandishi ya mwezi mmoja kabla ya kipindi cha Mkataba kuisha.
- (b) Kama Mpangaji hatakabidhi eneo hilo kama walivyokubaliana basi Mwenye eneo ana haki ya kumtoa kwa kutumia Dalali yeyote bila amri yoyote ya Mahakama.
- (c) Mgogoro wowote utatokea kuhusiana na Mkataba huu, basi mgogoro huo utatambuliwa kufuatana na sheria za nchi.

Mkataba huu umeshuhudiwa na wahusika kwa kutia sahihi zao katika namna na katika tarehe, mwezi na mwaka unaoonekana hapa chini.

**UMESAINIWA na KUTOLEWA na
JAPHARI MURRO** ambaye amekubaliwa
Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam
Leo 25 mwezi 09 mwaka 2025.



.....
MWENYE ENEO

**UMESAINIWA na KUTOLEWA
Na TARMALS AGRO LIMITED**
ambaye amekubaliwa
Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam
Leo 25 mwezi 09 mwaka 2025.



.....
MPANGAJI

SHAHIDI;

JINA DANIEL SIMON
.....

SAHIHI 

ANWANI 105269 DSM
.....

KAZI WAKILI
.....

